UFANISI MARADUFU WA DOUBLE MERIT

DARASA LA SABA - MWAKA 2018

SN:T1E202

KISWAHILI:
SEHEMU YA KWANZA:
LUGHA

Muda: Saa 1 Dak. 40

SOMA KWA MAKINI MAAGIZO YAFUATAYO

1. Umepewa kijitabu hiki cha maswali na karatasi ya kujibu. Kijitabu hiki kina maswali 50.
2. Ikiwa utataka kuandika chochote ambacho si jibu andika katika kijitabu hiki.
3. Ukishachagua jibu lionyeshe katika **KARATASI YA MA JIBU** na wala si katika kijitabu cha maswali.

JINSI YA KUTUMIA KARATASI YA MAJIBU

4. Tumia penseli ya kawaida.
5. Hakikisha kwamba yafuatayo yameandikwa katika karatasi ya majibu: -

   NAMBARI YAKO YA MTIHANI
   JINA LAKO
   JINA LA SHULE YAKO

6. Kwa kuchora kistari katika visanduku vyenye nambari zinazokuhusu, onyesha namba yako kamili ya mtihani (yaani nambari ya shule na zile namba tatu za mtahiniwa) katika sehemu iliyotengwa mwanzoni pa karatasi ya majibu.
7. Usitie alama zozote nje ya visanduku.
8. Iweke safi karatasi yako ya majibu.
9. Kwa kila swali 1-50 umepewa majibu manne. Majibu hayo yameonyeshwa kwa herufi A, B, C, D. Ni jibu MOJA tu kati ya hayo manne ambalo ni sahihi. Chagua jibu hilo.
10. Kwenye karatasi ya majibu, jibu sahihi lionyeshwe kwa kuchora kistari katika kisanduku chenye herufi uliyochagua kuwa ndilo jibu.

DOUBLE MERIT

Mfano:
Katika kijitabu cha maswali:
<u>Kutoka swali 16 - 30 chagua jibu sahihi.</u>

20. Kifaa cha mhunzi cha kushikia vyuma anavyofua huitwaje ?

    A. Timazi
    B. Jiriwa
    C. Mvukuto
    D. Utepe

Jibu sahihi ni B.

20. [A] [B] [C] [D] **21.** [A] [B] [C] [D] **22.** [A] [B] [C] [D] **23.** [A] [B] [C] [D]

Katika visanduku vinavyoonyesha majibu ya swali namba 20 , kisanduku chenye herufi B ndicho kilichochorwa kistari.

11. Chora kistari chako vizuri. Kistari chako cheusi kisijitokeze nje ya kisanduku.
12. Kwa kila swali, chora kistari katika kisanduku kimoja tu kati ya visanduku vinne ulivyopewa.

Kitabu hiki cha maswali kina kurasa 7 zilizopigwa chapa.

FUNGUA KURASA

Soma kifungu kifuatacho. Kina nafasi* 1 *hadi* 15. *Kwa kila nafasi, chagua jibu lifaalo zaidi kati ya yale manne uliyopewa kujazia nafasi zilizoachwa wazi.

Ajali ____1____ barabarani ____2____ husababishwa na ____3____ wa ____4____ wa madereva barabarani. Ni muhimu kwa watumiaji wote ____5____ barabara ____6____ sheria au ____7____ ili waokoe maisha. Vifo ____8____ bila shaka hupungua tukiwa waangalifu.

1. A. ya B. vya C. za D. cha
2. A. angalau B. aghalabu C. kwa nadra D. angaa
3. A. wingi B. uendeshaji C. utomvu D. utovu
4. A. umakinifu B. uangalifu C. nidhamu D. nidhamu
5. A. wa B. kwa C. katika D. kando ya
6. A. kufwata B. kutazama C. kufuata D. kupuuza
7. A. kanuni B. ardhi C. maigizo D. polisi
8. A. zinazotokea B. vinazotokea C. vitokeazo D. vitokeavyo

[illegible] ____9____ [illegible] nidhamu ya dini. Ni ____10____ kusema ____11____, iwe kwa kuepuka adhabu au kupata kitu fulani. Kosa ni kosa. Hakuna kosa ____12____. Kila kosa huwa na matokeo. Ni ____13____ kufikiria matokeo ya kudanganya ____14____ wahenga walisema ____15____.

9. A. Kutokana B. Kuendana C. Kutoka D. Kusikilizana
10. A. thambi B. [illegible] C. dhambi D. kasoro
11. A. uwongo B. [illegible] C. wongo D. uhongo
12. A. ndogo B. kidogo C. mdogo D. dogo
13. A. mzuri B. vyema C. vema D. kuzuri
14. A. kwa sababu B. kama C. kwa kuwa D. kwa vile
15. A. mtoto hutazama mzazi B. mwana wa nyoka ni nyoka
    C. upandacho mchongoma ujue utashuka D. upandacho ndicho uvunacho

Kutoka swali la 16 mpaka 30, chagua jibu lililo sahihi.

16. *Kanusha.*
Kucheza kwake kungemsaidia.
A. Kutocheza kwake kungemsaidia.
B. Kucheza kwake kusingemsaidia.
C. Kutocheza kwake hakungemsaidia.
D. Kutocheza kwake kusingemsaidia.

17. *Kikembe cha nzige* ***si***
A. maige
B. tunutu
C. funutu
D. matutu

18. Silaha ya kizamani ni ipi?
A. Topito
B. Kombeo
C. Bunduki
D. Manowari

19. Watu wanapoagana kwa muda mrefu sana huagana
A. buriani
B. enda salama
C. kwaheri
D. inshallah

20. *Chagua kivumishi na kielezi.*
A. Mwalimu, mfupi
B. Chaki, mrembo
C. Kirefu, kwa upole
D. Maji, furaha

21. *Chagua wingi.*
Ua la waridi liko uani.
A. Maua ya waridi yako mauani.
B. Nyua za waridi ziko nyuani.
C. Maua ya mawaridi yako nyuani.
D. Maua ya mawaridi yako mauani.

22. Nenda ukam____ mtoto kitandani.
A. laze
B. lishe
C. lalishe
D. lazie

23. Maneno kama rinda na linda ni vitate, kaa na panda ni
A. vitenzi
B. vitawe
C. visawe
D. vibadala

24. Ndugu mdogo huitwaje?
A. Umbu
B. Dada
C. Kaka
D. Mnuna

25. Ukubwa wa mwizi ni jizi, udogo wa mtoto ni
A. toto
B. kijitoto
C. kitoto
D. vitoto

26. *Chagua kiwakilishi cha nafsi ya pili wingi.*
A. Nyinyi
B. Wao
C. Wewe
D. Sisi

27. *Chagua ki ya masharti.*
A. Kidovu kimekimbia.
B. Kiki akipita tutafurahi.
C. Amekuwa akisoma.
D. Kiatu kingine kimeraruka.

28. Kupiga mafamba ni
A. kuenda mbio.
B. kunywa maji.
C. kudanganya.
D. kufa.

29. Majira ya jua kali hadi mito hukauka na mazao kukosekana husababisha
A. mchoo
B. masika
C. ukame
D. mafuriko

30. *Andika kinyume.*
Vijana na wasichana wanalia.
A. Wasichana na vijana wanalia.
B. Wazee na wavulana wanalia.
C. Wazee na wavulana wanacheka.
D. Kijana na mama wanacheka.

<u>Soma kifungu hiki kisha ujibu maswali 31 hadi 40.</u>

Asilimia kumi ya mifugo wa baba ndiyo pekee iliyobaki. Walibaki ng'ombe arubaini na kondoo kadhaa. Ukame ulikuwa umeangamiza mimea, mifugo na hata wanyama wa porini. Mvua iliponyesha hatimaye, maji yalikuwa yamemwagika, hayazoleki.

Janga la vumbi, joto lililokithiri, vifo, kiu yenye kuangamiza na madhira ya aina zote yalitusakama kama kibanzi cha kuni. Mvua ilinyesha kidogo kidogo mwanzoni lakini baadaye iliongezeka. Majani na mimea mingine ilipamba mandhari yakawa na mkeka wa kijani. Jamii za wafugaji, yetu ikiwemo, zilikuwa zimekata shauri kubadili mkondo wa maisha. Tulilima mashamba ambayo awali tuliyaona kama kutia ardhi vidonda! Ama kweli, lisilo budi hubidi.

Baba yangu alitamauka kufuga kundi zima la mifupa na ngozi. Aliuza magofu yote ya wanyama na fedha alizopata akanunulia seng'enge na vigingi vya kujengea ua kuzunguka shamba letu lote. Tulitumia michemu na mitaimbo kuchimbia mashimo ili tujenge ua. Majirani nao walilima lakini mimea iliharibiwa na mifugo na wanyamapori wengine. Nafasi ya kuupa ukata kisogo ikatokea. Walimwomba baba awauzie seng'enge na vigingi pia.

Baba alitumia akiba yake akasafiri mjini kwenye kiwanda cha baniani akaleta seng'enge, misumari, nyundo, majembe, mipini na rato kwa bei ya jumla. Naye akawauzia wanakijiji kwa bei ya kuruka. Mifuko yake ilifurika. Hivyo ndivyo milango ya heri ilivyofunguka na kijiji chetu sasa kinajulikana kwa ukulima wa mimea. Nikamilishapo masomo yangu chuoni, bila shaka nitaendeleza biashara za baba.

Maamuzi mengine, ingawa machungu, huzaa matunda kochokocho hatimaye.

31. Kulingana na mwandishi, ng'ombe waliobaki
    A. walikuwa wachache sana
    B. walikuwa chini ya nusu ya idadi ya awali
    C. walikuwa kumi
    D. waliongezeka baadaye

32. Ni viumbe gani hawajatajwa kuuliwa na ukame?
    A. Ng'ombe
    B. Kondoo
    C. Wanyamapori
    D. Nyuni

33. Kukata shauri maana yake ni
    A. kuamua
    B. kukata kesi
    C. kubadili
    D. mkondo maisha

34. Jamii ya mwandishi
    A. ilisifu sana kilimo cha mimea
    B. ilikuwa ya wawindaji
    C. ilikuwa ya wafugaji
    D. ilikuw ana mali mengi awali

35. Sentensi gani sahihi?
    A. Familia ziliamua kulima kwa hiari
    B. Jamii ililazimika kulima
    C. Mwandishi ni mfanyabiashara
    D. Nafasi ikitumiwa vizuri huleta hasara

36. Kifaa cha kuchimbia vishimo ya vigingi ni
    A. jembe
    B. seng'enge
    C. nyundo
    D. mchemu

37. Kuupa ukata kisogo ni
    A. kusema kwaheri kwa ukata
    B. kuanza kilimo
    C. kupata mali
    D. kuuza mifugo wakondefu

38. Mtaji wa biashara ya vifaa vya kilimo
    A. ulitokana na kuuza mifugo na akiba
    B. ulitokana na kilimo
    C. haukutosha
    D. ulitokana na mkopo

39. Mwandishi
    A. ni mwanachuoni
    B. anasoma shule ya upili
    C. amekamilisha masomo
    D. hana nia ya kufanya biashara

40. Bei ya kuruka
    A. ni ya juu sana
    B. ni hafifu
    C. ni ya rejareja
    D. ni bahasa

DOUBLE MERIT

Soma taarifa ifuatayo kisha ujibu swali la 41 hadi 50.

Abdi alikuwa kijana aliyehitimu miaka kumi na mitatu. Alikuwa mtiifu na mnyenyekevu kwa wazazi na walimu wake. Aliwapigia magoti wakubwa wake kwa kuwa alielewa heshima si utumwa. Alikuwa na maadili na mara nyingi alipigiwa mfano kijijini na hata shuleni. Licha ya hayo alikuwa mwenye bidii ya mchwa.

Alijikaza vilivyo ili aweze kufaulu katika mitihani yake. Alikuwa akifuata maagizo ya babake aliyekuwa akila jasho lake. Bila shaka mtoto akibebwa mgongoni hutazama kisogo cha mama yake. Kwake, vitabu vilikuwa rafiki wa kufa kuzikana. Baba yake pia hakuchelewa kumkosoa iwepo alifanya makosa.

Abdi alikataa katakata kuandamana na watu waliokuwa na tabia zilizonuka fe! Hata hivyo, alishauri wengine kuacha utundu na uzumbukuku ambao uliwafanya kushika mkia darasani. Kama ilivyo desturi yao waliyapa mawaidha yake kisogo. Yote yalikuwa kama kumtafuta paka mweusi kwenye giza totoro. Laiti wangalijua majuto ni mjukuu, wangalishikilia mawaidha hayo na kuyang'ang'ania ng'ang'anu ng'ang'anu.

Kijana wetu hakuchelea kuuliza maswali darasani kwani alielewa kuuliza .... wananyosema wahenga. Vile vile anayeuliza ana la kujifunza. Naye alijifunza kulingana na maswali na makosa aliyokosolewa.

Pale shuleni, Abdi alikutana na kijana mmoja aliyemchukulia kama rafiki yake. Walisoma pamoja, waliendea maakuli pamoja na kucheza pamoja. Hakika hata kila mitihani yote waliibuka washindi.

Siku moja rafiki yake aliyekuwa wa dhati alimkuta amejilaza kitandani. Kwa kuwa alimfaa wakati wa mvua na wakati wa jua alitaka sana kujua sababu yake ya kulala mchana. Alimwelezea kuwa aliugua homa na mafua. Bila kuchelea alimpa unga mweupe akimwambia aurambe ili apate nafuu. Ukweli ni kwamba afya yake ilirudi vizuri baada ya siku chache. Hakujua kuwa maisha yake yalianza kupata mwanya. Kumbe unga ule ulikuwa mihadarati. Aliendelea kuuramba kwa kuwa mazoea yalimshika. Masomo ya kijana wetu yalianza kudorora.

Tabia zake ziliharibika na nia yake ya masomo ikawa nzito. Mwalimu mkuu na wengine walimshauri kuhusu utundu na uzembe lakini wapi! Rafiki yake tu ndiye aliyekuwa akimpongeza kwa utundu wake.

Hatimaye Abdi alitumwa nyumbani. Baada ya mama mzazi kumsaili, iligundulika kuwa alikuwa anatumia mihadarati. Chanzo kilikuwa rafiki mnafiki. Aliamua kutengana naye kama ardhi na mbingu baada ya kurudi shuleni. Rafikiye alifukuzwa shuleni. Tangu siku hiyo hajawahi mtia machoni tena.

41. Abdi alikuwa mnyenyekevu kwa
   A. walimu wake
   B. wazazi wake
   C. wakubwa wake
   D. rafiki zake

42. Walimu na wazazi wengi kijijini waliwashauri watoto wao kuwa kama Abdi kwa nini?
   A. Alikuwa namba moja
   B. Alikuwa na maadili
   C. Alikuwa na rafiki mzuri
   D. Alikataa kuandamana na watu wengi

43. Baba mtu alikula jasho lake kumaanisha
   A. alitegemea kazi yake ngumu kupata mapato
   B. alitegemea Abdi kupata mapato
   C. alikaa bila kazi
   D. alikuwa na kazi ya kifahari

44. Kulingana na habari '*kumnaruta paka mweusi gizani*' imelinganishwa na
   A. [illegible]bia ya Abdi
   B. tabia ya rafiki [illegible]
   C. ugumu wa wengine [illegible] mashauri ya Abdi
   D. kutofuata maagizo [illegible]

45. *Kamilisha.* Kuuliza ....
   A. ni kutaka kujua
   B. sana ni kutaka majibu mengi
   C. ni kutaka kujifunza
   D. si ujinga

46. Nini ilikuwa sababu ya Abdi kujilaza kitandani?
   A. Alikuwa amcramba unga mweupe
   B. Alipumzika kwa kusoma sana
   C. Aliugua homa bila mafua
   D. Aliugua mafua na homa

47. [illegible] kikutacho ki nguoni mwako [illegible] kana vipi katika habari?
   A. Rafiki wa Abdi kumletea Abdi mihadarati na kumharibu
   B. Shule kumfukuza rafiki wa Abdi
   C. Abdi kukataa katakata kujiunga na watu waliokuwa na tabia zilizo[illegible]
   D. Rafiki wa Abdi kumsaidia wakati wa mvua na wakati wa jua

48. Unga uliopewa kijana wetu bila [illegible] ulikuwa ni
   A. sigara
   B. dawa ya homa
   C. mihadarati
   D. ugoro

49. Nini [illegible] [illegible] kuwa [illegible]?
   A. [illegible]
   B. Mihadarati
   C. Watu waliokuwa na tabia [illegible]
   D. Tabia zake Abdi zilizo[illegible]

50. [illegible] rafiki wa Abdi [illegible] walikutana mara ngapi?
   A. Mara kwa mara
   B. Mara nyingi wakicheza pamoja
   C. Hatujaambiwa
   D. Hawajawahi kutana katu